# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## OFISI YA WAZIRI MKUU

## TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

# MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE ZA SEKONDARI ZA SERIKALI TANZANIA

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI –**
**TAMISEMI**

**Namba za Simu**

**Mkuu wa Shule: 0782 972 370**

**Makamu Mkuu wa Shule: 0755247151**

**Matron: 0717 791 433**

**Shule ya Sekondari Msalato,**
**S.L.P. 933,**
**Dodoma.**

**Tarehe. ....................**

**Mzazi/Mlezi wa Mwanafunzi ………….**
**……………………………………………..**
**S.L.P ……………………………………..**
**…………………………………………….**

**Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO KATIKA SHULE YA SEKONDARI MSALATO HALMASHAURI YA JIJI LA DODOMA MKOA WA DODOMA JULAI ........**

**1.** Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka **..................** na atasoma tahasusi ya ………………….

Shule iko kilomita kumi (10km), kaskazini mwa mji wa Dodoma, ukifuata barabara kuu iendayo Kondoa-Arusha. Usafiri wa daladala unapatikana kituo cha daladala cha Machinga panda daladala iendayo Veyula/Msalato shuka kituo cha Bible, nauli ni sh. 700/= kwa pikipiki ni shilingi 10,000/= na kwa bajaji ni shilingi 15,000/= tu, wanaotokea Arusha kuja Dodoma shuka kituo cha Msalato Bible.

Mwisho wa kuripoti ni saa 12.00 jioni. Ukikwama piga simu hiyo hapo juu kwa ushauri na maelekezo zaidi.

Muhula wa Masomo unaanza tarehe **..............................** hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni tarehe . . . . . . . . . . . . Mwisho wa kuripoti ni tarehe ............ Endapo hutapenda kujiunga na shule hii toa taarifa ya maandishi ndani ya

hizo wiki mbili. Hali kadhalika, epuka usumbufu kwa kufika shuleni hapa kwa **nyaraka na jina la mtu mwingine**! Njoo na barua hii kwa utambulisho. Omba kuonana na mwalimu wa zamu ambaye atakupokea na baadae kukuelekeza kwa 'boarding master' wa shule kwa ajili ya kukabidhi vifaa vilivyoelekezwa hapa chini.

## 2. Mambo muhimu ya kuzingatia:-

### 2.1 a) Sare za Shule

i) Mashati meupe mawili (2) yenye mikono mifupi na mfuko upande wa kushoto.
ii) Sketi za darasani, mbili (2) kitambaa cha suti esteem namba moja (1) **bluu bahari** (light blue) yenye marinda yanayoangalia upande mmoja na yanayolingana kati ya 13 - 15, **na iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu (IGUSE KIATU).**
iii) Sketi za nje ya darasa, mbili (2) kitambaa cha suti esteem namba moja (1) **damu ya mzee** (maroon) mshono wa solo ambayo siyo pana sana, **iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu** (IGUSE KIATU).
iv) T-sheti 2 vazi la nje ya darasa yenye kola (form six).
v) Sweta 2 nyeusi zenye shingo ya V mbele.
vi) Tai ndefu ya pundamilia rangi ya light blue na dark blue.

**2.1 b) KWA <u>WANAFUNZI WAISLAMU</u>:**

i) Nusu kanzu nyeupe mbili (2) zenye mikono mirefu.
ii) Hijabu mbili nyeupe na vikofia vyeupe
iii) Sketi za darasani, mbili (2) kitambaa cha suti esteem namba moja (1) **bluu bahari** (light blue) yenye marinda yanayoangalia upande mmoja na yanayolingana kati ya 13 - 15, **na iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu** (IGUSE KIATU)
iv) Sketi za nje ya darasa, mbili (2) kitambaa cha suti esteem namba moja (1) **damu ya mzee** (maroon) mshono wa solo ambayo siyo pana sana, **iwe ndefu kufikia kifundo cha miguu** (IGUSE KIATU)
v) Hijabu mbili za damu ya mzee (maroon) na vikofia vyake
vi) T-sheti 2 vazi la nje ya darasa **RANGI YA KIJIVU** iliyokolea yenye kola (form six)
vii) Sweta 2 nyeusi zenye shingo ya V mbele.



**<u>SARE YA DARASANI</u>**



**<u>VAZI LA NJE YA DARASA</u>**

### 2.2 Mahitaji mengine muhimu ambayo mwanafunzi anapaswa kuja nayo shuleni:-

a) Daftari kubwa “counter book Q4” zisipungue 12,kalamu, penseli, rula, mkebe wa Hisabati n.k

b) **Ream (A4)** ya Karatasi Mbili (2) aina ya ”Double A” kwa mwaka;

c) Viatu vya shule vya ngozi nyeusi vya kufunga na kamba jozi 2, kiwi na brashi yake na **soksi nyeupe ndefu zisiwe na weusi kwenye unyayo angalau jozi 2**. Pia aje na raba nyeupe jozi moja kwa ajili ya michezo.

d) Track Suit **rangi moja.** Iwe nyeusi au bluu iliyokolea (dark blue) lenye mistari mweupe pembeni kwa ajili ya mazoezi na kuzuia mbu na baridi anapojisomea usiku.

e) Vifaa vya kulia chakula kama sahani/ container, bakuli, kikombe, kijiko na chombo safi cha kuhifadhia maji ya kunywa.

f) Mto, shuka (Pink) 2 na foronya (Pink) 2 na blanketi moja zito. Aje na taulo na jozi moja ya kitenge au khanga, Net (chandarua) ya futi 3 ½ rangi nyeupe, vibanio vya nguo seti moja. **Nguo za nyumbani haziruhusiwi kabisa.**

g) Vifaa vya usafi binafsi kama sabuni, mswaki na dawa, ndala za kuogea bata au umoja, mafuta ya mgando ya kujipaka mwilini, taulo za kike (pads), toilet paper' n.k . **Perfume/Spray haziruhusiwi kabisa wala mafuta yenye harufu kali.**

h) Nguo za ndani za kutosha kama chupi, shimizi/gagulo, skin tight, sidiria n.k ziwe nyeupe au nyeusi tu.

i) Tochi na betri/Taa ndogo ya jua na sanduku imara (**trunker)**.

j) Ndoo ya kuogea na kuhifadhi maji ya lita 10

k) Nguo za kulalia (night dress) rangi nyeupe au nyeusi, nyepesi zinazoangaza.

l) Viatu vya wazi vya kimasai (culture) kwa ajili ya kushindia.. Ndala za umoja au bata zitatumika bafuni na maliwatoni tu.

m) Vitabu vya masomo ya tahasusi husika (*nunua vitabu vya Taasisi ya Elimu (TIE)*);

n) **Dissecting Kit** kwa wanafunzi wa tahasusi (combination) ya PCB

o) Scientific Calculator kwa wanafunzi wa tahasusi zote.

p) Godoro size 6 x $2^{1}/_{2}$. Aidha, godoro linaweza kukodishwa shuleni kwa gharama ya **Shilingi 10,000.00** kwa mwaka; **Tsh. 5,000 kwa muhula**.

q) Vifaa vya usafi;

Wanafunzi wanaosoma **PCB** waje na **Sabuni ya maji** lita tano aina ya **DEXI au CARE LINE** pamoja na "**hard broom"** moja imara. Wanafunzi wanaosoma **PCM** waje na **mopper complete seti** moja na **squeezer** moja na Wanafunzi wanaosoma **HGL** waje na **soft broom, chelewa ndefu yenye mpini** na **squeezer** moja viwe imara. **PMCs** waje na **Panga, Brash ya kusafishia choo**, **Jembe na mpini wake**.

**ANGALIZO**:

a) Mwanafunzi asije na mizigo au begi kubwa shuleni, aje na Tranka moja imara.

b) Hairuhusiwi mwanafunzi kutembelewa na wageni wakati wote atakaokuwapo shuleni ISIPOKUWA kwa wito maalum wa Mkuu wa Shule. Siku ya kuwaona wanafunzi itatangazwa rasmi.

c) Ni marufuku mwanafunzi kuja na nguo za nyumbani, mwanafunzi atarudishwa nyumbani mara moja endapo atakiuka kipengele hiki.

### 2.2 Michango mbalimbali ya uendeshaji wa shule Tsh 80,000/=

Utatakiwa kulipa michango kwa mchanganuo ufuatao:-

| Na | Aina ya Mchango | Kiasi |
|---|---|---|
| 1 | Mchango wa uendeshaji wa shule | 65,000 |
| 2 | Tahadhari | 5,000 |
| 3 | Nembo | 5,000 |
| 4 | Kitambulisho cha shule | 5,000 |
|  | **Jumla** | **80,000** |

Malipo yote yalipwe kupitia **Benki ya NMB** tawi lolote au wakala yeyote nchini kwa kupitia akaunti namba **50501100161** yenye jina **MSALATO SECONDARY SCHOOL ACCOUNT.** Stakabadhi zote za malipo (bank pay in slip) ziletwe shuleni zikiwa na jina kamili la mwanafunzi, kidato na tahasusi yake.

**ZINGATIA**

Malipo yote yalipwe benki, shule haitahusika na malipo yoyote yatakayo fanywa bila kupitia benki.

## 3. Sheria na Kanuni muhimu za Shule

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa Sheria ya Elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyo rekebishwa kwa Sheria Na. 10 ya mwaka 1995. Aidha, inazingatia miongozo yote inayotolewa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia yenye dhamana ya elimu na Ofisi ya Rais – TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji wa elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo ambayo yanafafanuliwa kwa maandishi na utapewa nakala yake mara baada ya kuripoti shuleni. Mambo hayo ni pamoja na;

### 3.1 Sheria na Kanuni za Shule

i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.;
ii. Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule;
iii. Kushiriki kwa kikamilifu masomo ya usiku( Preparation);
iv. Kuwahi katika kila shughuli za shule utakazopewa;
v. Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelekezo ya kuwepo ndani na nje ya shule ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii;
vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule;
vii. Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa;
viii. Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote;
ix. Kutunza mali za shule;
x. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki vifaa vyenye ncha kali na dawa bila idhini ya daktari; na
xi. Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini wala kumshawishi mwanafunzi mwenzake kubadili dini wawapo shuleni.

**MUHIMU:**

- ❖ **Mwanafunzi hapaswi kuja na simu shuleni kwa namna yoyote ile, na hakuna mtumishi anayeruhusiwa kutunza simu ya mwanafunzi;**
- ❖ **Mwanafunzi awapo shuleni atatakiwa kulala kwenye Bweni alilopangiwa na kitanda alichopangiwa. Ni marufuku mwanafunzi kulala kitanda kimoja na mwenzake au kuishi kwenye Bweni ambalo hakupangiwa. Kitanda kimoja kitatumika na mwanafunzi mmoja tu;**

- **Mwanafunzi ataruhusiwa kurudi nyumbani kwa ruhusa na kibali maalum toka kwa Mkuu wa Shule. (Msiba au Ugonjwa**).

**3.2 Makosa yatakayosababisha Mwanafunzi kufukuzwa Shule ni pamoja na:**

i. Wizi;
ii. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro;
iii. Kugoma na kuhamasisha mgomo;
iv. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla;
v. Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu au mtu yeyote yule;
vi. Mwanafunzi haruhusiwi kusuka . Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni;
vii. Kufuga ndevu;
viii. Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya dawa za kulevya;
ix. Uvutaji wa sigara;
x. Uasherati, mahusiano ya jinsi moja, kuoa au kuolewa;
xi. Kupata ujauzito au kutoa mimba;
xii. Kusababisha mimba;
xiii. Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi;
xiv. Kwenda kwenye nyumba za starehe na nyumba za kulala wageni;
xv. Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule;
xvi. Kudharau Bendera ya Taifa;
xvii. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu; na
xviii. Uharibifu wa mali ya umma kwa makusudi.

**4. Viambatisho na Fomu Muhimu**

i. Fomu ya Uchunguzi wa Afya (Medical Examination Form) ambayo itajazwa na Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali;
ii. Fomu ya Maelezo Binafsi kuhusu Historia ya Mwanafunzi/Mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai;
iii. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yanayotolewa na shule; na
iv. Picha nne (4) za wazazi na ndugu wa karibu wa mwanafunzi wanaoweza kumtembelea mwanafunzi shuleni pamoja na Namba zao za Simu.

**MUHIMU**

Baada ya kupakua (download) fomu hii, tafadhali jaza jina la mwanafunzi na anwani yako pamoja na tahasusi aliyochaguliwa kusomea hapa Sekondari ya Msalato. Hakikisha unajaza tahasusi (combination) aliyopangiwa na serikali. Taarifa hizi zijazwe kwenye ukurasa wa kwanza.Mwanafunzi atakaporipoti shuleni aje na fomu hii pamoja na **result slip ya kidato cha nne**. Mwanafunzi aje na nakala ya **Cheti cha kuzaliwa** (Birth Certificate).
Mwanafunzi aje na kadi ya **bima ya afya**.

Tafadhali soma kwa makini maelezo/ maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

**KARIBU SANA MSALATO SEKONDARI**

HEADMISTRESS P. O. BOX 933 DODOMA MSALATO SECONDARY SCHOOL

MWASITI MSOKOLA
**Mkuu wa Shule**

**NB: Kwa siku za hivi karibuni kumekuwa na utapeli (wizi kwa njia ya mitandao). Baadhi ya wazazi wamekuwa wakitumiwa ujumbe mfupi au kupigiwa simu na watu wanaojitambulisha kama walimu na kuwafahamisha kuwa mtoto wa mzazi husika mbaye ni mwanafunzi ni mgojwa na yuko mahututi hivyo mzazi atume pesa. TAFADHALI UPATAPO UJUMBE WOWOTE KUHUS MWANAFUNZI/MTOTO WAKO USITUME CHOCHOTE, NI VEMA UKAWASILIANA NA UONGOZI WA SHULE KUPATA UKWELI WA TAARIFA HUSIKA KWA NAMBA ZIFUATAZO: -**

- **Mkuu wa shule: 0782 972 370 (Mwl Mwasiti Msokola)**
- **Makamu Mkuu wa Shule: 0755247151( Mwl Rhoda Mbalani)**
- **Mwandamizi Taaluma: 0784 405 210 (Mwl Joshua Nasari)**
- **Mwandamizi Malezi: 0757 408486 (Mwl Rhoda Mzunde)**

## SHULE YA SEKONDARI MSALATO
## FOMU YA KUKUBALI SHULE

### A. SEHEMU YA MWANAFUNZI

1. Mimi (Majina kamili) ………………………………………………………………..
   Nimekubali kuingia kidato cha …………… katika Shule ya Sekondari Msalato Dodoma kuanzia tarehe ………………….. hadi nitakapomaliza kidato cha …………
2. Naahidi kwamba nitatii sheria za Shule na kushiriki katika shughuli zote za shule kikamilifu kulingana na ratiba.
3. Tarehe ya kuzaliwa………………………..Kijiji/Mtaa…………………………………..
   Tarafa…………………………………….. Wilaya ………………………………...
   Shule unakotoka ……………………………………..Namba yako ya mtihani……
4. Kituo cha gari (Bus) au Gari la Moshi kilichopo karibu na nyumbani kwako ………………..
5. Nikimaliza kusoma shule ningependa kufanya kazi ifuatayo ………………………

Saini ya mwanafunzi ……………………. Tarehe ………………………………...

### B. SEHEMU YA MZAZI AU MLEZI

1. Mimi (majina kamili) ………………………………… simu……………………
   ninakubali mtoto wangu asome katika Shule ya Sekondari ya Wasichana Msalato kuanzia kidato cha …………hadi atakapomaliza kidato cha ……………
2. Jina kamili la Mama ………………………………………………
   Kazi ya Mama……………………………………Simu…………………………….
3. Kazi ya Baba …………………………………….. Simu…………………………….
4. Anwani ya Mzazi/Mlezi ……………………………..........................................................
5. Wafuatao ni Ndugu zake ninaowatambua wanaweza kumsaidia wakati wa dharura

| Jina kamili | Mahusiano | Anakoishi | Simu yake |
|---|---|---|---|
| (i)…………………… | …………….. …… | ……………………. | …………… |
| (ii)…………………… | …………..………. | ……………………. | …………… |
| (iii)……………………. | ……………………… | ………………….. | …………… |
| (iv)……………………… | ……………………. | …………………. | …………….. |

6. Dini ya Mtoto ni: Mkristo/Muislam **(kata lisilohusika)**
7. Ripoti zote za maendeleo ya mwanafunzi ziwe zinatumwa kwa .......................................................

Sani ya Mzazi/Mlezi………………………………. Tarehe ……………………

***MSALATO SECONDARY SCHOOL***
***FORM FOR STUDENTS MEDICAL EXAMINATION***

To be completed by a Medical Officer

……………………………………(Insert name of **the** Government Medical Institution)

Name of Student …………………………………………. Form …… Year……….

Age ……………………………………    Sex…………………………………..

Blood count ……………………………………………………………………

Stool ……………………………………………………………………………

Urine ……………………………………………………………………………

T. B. Test ………………………………………………………………………

Eyes ……………………………………………………………………………

Ears ………………………………………………………………………………

Chest ……………………………………………………………………………

Spleen ……………………………………………………………………………

Abdomen ………………………………………………………………………

Teeth ……………………………………………………………………………

Additional information:- (***e.g. pregnancy, physical defects, infections, psychological disorder, chronic or family diseases)***

…………………………………………………………………………………………

………………………………………………………………………………………

**I certify that above pupil is fit to continue with studies in Secondary School for four years.**

Name of Medical Officer ……………………………Signature ……………………

Designation …………………………………..
Station & Official Stamp……………………… Date …………………………..

***Sharti mtoto apimwe kikamilifu kabla ya daktari kujaza fomu hii. Ikigundulika kuwa daktari alijaza fomu hii bila vipimo kufanyika, wahusika watachukuliwa hatu za kisheria na za ukiukaji wa haki za binadamu.***